# LIJUE
# KANISA LA KRISTO

**NA**
**ROD RUTHERFORD**



Kanisa la Kristo siyo dhehebu lililoanzishwa na mwanadamu na wala siyo sehemu ya chama cha dini kilichoanzishwa na wanadamu. Kanisa hili chimbuko lake ni Mbinguni lilitokana na mawazo ya Mungu na hapa duniani lilianzishwa katika mji wa Yerusalemu Siku ya Kwanza ya Pentekoste kufuatia ufufuo wa Bwana wetu Yesu Kristo (Efe. 3:8-11; Mdo. 2). Badala ya kujishughulisha na madhehebu waumini wa Kanisa la Kristo wanakubaliana na kuamini kwamba Yesu Kristo anawaunganisha katika maombi wanakuwa kitu kimoja katika damu ya Yesu na Kanisa, Yn. 17:20-21; Efe. 4:4-6; Mdo. 20:28.

Msingi wa Kanisa la Kristo ni Yesu Kristo mwenyewe (1 Kor. 3:11). Jengo huwa imara kutokana na msingi, ni sawa kabisa na Kanisa. Kama Kanisa limejengwa na mwanadamu kwa imani yake bila Yesu, litaanguka. Ni Yesu Kristo peke yake anayeweza kujenga Kanisa kwa sababu yeye ni Mwana wa Mungu anayeishi Mt. 16:13-19.

Imani ya Kanisa la Kristo ni kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu anayeishi (Mt. 16:16). Yesu Kristo kabla ya kupaa kwenda Mbinguni aliwaambia mitume wake "*nendeni ulimwenguni mwote mkawafundishe mataifa yote na mkiwabatiza katika jina la Baba, na la Mwana, na Roho Mtakatifu, wafundisheni kulishika neno langu kama nilivyowaamuru na nitakuwa nanyi siku zote mpaka mwisho wa dunia, amina*" Mt.

28:19-20. Mitume na wainjilisti wa karne ya kwanza chini ya usimamizi wa Roho Mtakatifu waliandika mafundisho ya Yesu Kristo, ambayo tunayo katika Agano Jipya. Hatuna sheria nyingine mafundisho haya yanatutosha hatuna haja ya kuyabadilisha mpaka hapo Yesu atakapokuja mara ya pili, (2 Tim. 3:16, 17).

Vigezo ambavyo vinatumiwa na Kanisa la Kristo ni vile vinavyopatika katika Agano Jipya katika (Mdo. 11:26) tunasoma “huko Antiokia ndiko kwa mara ya kwanza wafuasi waliitwa Wakristo”. Katika Warumi 16:16 “salimianeni ninyi kwa ninyi kwa ishara ya upendo salamu kutoka kwenu katika Makanisa ya Kristo”. Mt. 16:18, Yesu alisema, “Nitalijenga kanisa langu”. Neno lenyewe Kanisa la Kristo kwa ufupi lina maana Kanisa ni la Kristo kwa sababu ni mnunuzi na mjenzi na ukombozi unapatikana katika jina lake Mdo. 4:11-12.

Jinsi ya kuabudu katika Kanisa la Kristo imeonyeshwa wazi katika kitabu cha Agano Jipya. Yesu alisema “Mungu ni roho, na watu wataweza kumwabudu kweli kwa nguvu ya roho wake”. Siku ambayo wakristo wanaabudu ni Jumapili, Siku ya Kwanza ya juma ni Siku ya Bwana (Mdo. 20:7; 1 Kor. 16:2; Ufu. 1:10). Matendo yakufuata wakati wa kuabudu ni kuimba kuhubiri, kuomba, kutoa na kushiriki Chakula cha Bwana: Kol. 3:16; 1 Tim. 2:1-2; Mdo. 20:7-2; 2 Tim. 4:2; 1 Kor. 16:1-2.

Muziki utakaotumika katika ibada ni kuimba tu bila vyombo na hii ndiyo iliyoruhusiwa na mungu katika namna ya kufanya ibada katika Kanisa, Kol. 3:16; Efe. 5:19. Kuimba ni kwa kila Mkristo na siyo kuwapa nafasi watu wachache tu ambao ni wanakwaya. Hiyo haijaelezwa katika agano jipya kuhusu vyombo kama piano, magita, ngoma, havijaelezwa vitumike katika Agano Jipya hivyo kwa kuvitumia tunaenda kinyume na Mungu anavyotaka kama ilivyoandikwa kwamba ni dhambi, 2 Yn. 9-11; Ufu. 22:18-19.

Wakristo wa Kanisa la Kristo wanatoa kwa kadiri Mungu alivyowajalia, wanatoa Siku ya Kwanza ya Juma ambapo wamekusanyika na kuabudu 1 Kor. 16:1-2; 2 Kor. 9:7. Na mapato hayo yanatumika katika kazi ya Mungu kama vile kuhubiri injili na kuwasaidia wenye shida (Mk. 16:15; 2 Tim. 2:2; Gal. 6:10). Njia nyingine za kutafuta pesa katika kazi ya Bwana kwa kuanzisha gereji za kuuza vitu, minada, hoteli, na mengine mengi hayakuamuriwa katika kitabu cha Agano Jipya, hivyo hayatakiwi kufanywa bila mamlaka ya Kristo, 2 Yn. 9-11.

Kuhusu utaratibu wa uongozi katika Kanisa la Kristo unafuata utaratibu ambao ni rahisi ulioonyeshwa katika kitabu cha Agano Jipya. Yesu Kristo ndiye kiongozi Mkuu wa Kanisa Efe. 1:22-23; Kol. 1:18. Makao makuu ya Kanisa la Kristo ni Mbinguni ambako kiongozi mkuu yuko, Mdo. 1:9-11; 2:30-33. Wakristo katika kila jamii wanakusanyika pamoja na kumtumikia Mungu. Mdo. 20:6-7; 1 Kor. 1:1-2 kila mmoja wa sharika hizi ni “Kanisa la Kristo” na kwa ujumla ni “Makanisa ya Kristo,” Rum. 16:16. Kila Kanisa la Kristo linajitegemea chini ya Yesu Kristo ambaye ni kiongozi. Kanisa hili linaongozwa na “wazee,” Mdo. 14:23; “Maaskofu,” Fl. 1:1, “Wachungaji” Efe. 4:11; Tit. 1:5-7; 1 Pet. 5:1-4. Viongozi hawa ni lazima wawe na sifa kutoka kwa Mungu kabla ya kuanza kutumika katika kazi ya Bwana kama wazee, maandikoni ni watumishi, pia lazima

Wabarikiwe na Mungu kabla ya kuanza kazi.

Wainjilisti ni wahubiri wa injili, 2 Tim. 4:1-5.  Hawa watatangaza Injili chini ya wazee na watapeleka injili sehemu mbali mbali, (1 Tim. 1:3; Mdo. 8:5-40; 21:8-9).

Waumini wa Kanisa la Kristo ni wanaosikia neno la Mungu na kuamini Yesu Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu, na kutubu dhambi zao zote, na kukiri Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu anayeishi, na wabatizwe (kwenye maji) kwa msamaha wa dhambi, Rum. 10:17; Yn. 8:24; Mdo. 2:38; Rum. 6:4.  Na wote watakaobakia waaminifu mpaka kufa watapokea taji ya uzima (Ufu. 2:10; Gal. 6:7-9).

Biblia inaonyesha Kanisa moja ambalo ni Kanisa la Kristo (Efe. 4:4; Kol. 1:18).  Yesu ameahidi kulikomboa Kanisa Lake siku ya mwisho, Efe. 5:23.  Hakuna ukombozi utakaopatikana nje ya Kanisa la Bwana, na badala yake watahukumiwa katika moto wa milele, 2 The. 1:7-9.

Kwa nini usiwe mmoja wa watu wa Kanisa la Kristo?  Ili upate kurithi Ufalme wa Mbinguni.